TANGAZO LA SERIKALI NA. 356 la tarehe 10/05/2024

SHERIA YA MIPANGO MIJI
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1))*

## AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA VIWANDA MBEZI YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Eneo la Viwanda Mbezi ya Mwaka 2024.

Utangazaji wa eneo la upangaji
Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji(mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango

3. Mipango kina katika eneo lililotajwa chini ya aya 2 itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni.

## JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba DC68 yenye majira – nukta 522226.528MS, 9259125.703KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.12 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba DC62 yenye majira – nukta 522315.516MS,

9259199.358KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.28 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba DA779 yenye majira - nukta 522489.901MS, 9258969.128KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.12 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba DA557 yenye majira - nukta 522398.931MS, 9258901.548KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini -Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.18 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba YE817 yenye majira – nukta 522290.839MS, 9259042.087KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.09 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba YE820 yenye majira – nukta 522219.196MS, 9258988.71KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.09 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba YE821 yenye majira - nukta 522164.72MS, 9259061.52KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.09 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba YE818 yenye majira - nukta 522233.946MS, 9259116.058KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.012 hadi ulipoanzia”.

Dodoma — JERRY WILLIAM SILAA

25 April, 2024. — *Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*